# Kutafuta usawa kwa kila mtu

## Hali ya ubinadamu kuhusu uchimbaji madini ya dhahabu



www.iied.org



# Kutafuta usawa kwa kila mtu

Utawapata watu wa hali tofauti katika eneo lolote la uchimbaji madini ya dhahabu. Kwa kuwaangalia tu, wanaweza kuonekana tofauti — wanatumia zana tofauti, wanafanya kazi katika hali tofauti, na wanafanya kazi chini ya sheria tofauti. Endapo utaamini wanayosema wanahabari, huenda ukaamini kwamba tofauti zao ndio utambulisho wao, na kwamba hali yao inahusu mgogoro, uchafuzi wa mazingira na unyanyasaji.

Lakini ukiangalia vizuri utapata kuwa wana mambo mengi yanayowaunganisha zaidi ya ulivyowadhania, na kwamba hali yao ni ya muungano wa ubinadamu, maadili ya pamoja na matumaini ya umoja ya maisha mema. Kuanzia mwanajiolojia aliye afisini mwake hadi mchimba madini aliye katika migodi, na kuanzia afisa wa madini hadi kiongozi wa kijiji, wachimba madini wa kiwango cha juu, wa kiwango cha chini, na serikali, wote ni binadamu.

Wao ni kina baba, wana, mama, mabinti — wanaofanya kazi ili kukidhi mahitaji ya familia zao na kuwa na maisha bora ya baadaye, yao wenyewe na ya wapendwa wao.

Hii ndiyo hali ya ubinadamu kuhusu uchimbaji madini ya dhahabu.

## Mazungumzo tetezi

IKazi ya IIED katika uchimbanji wa kiwango cha juu cha chini huwezesha mazungumzo ya wadau wengi, hukuza maoni ya watu wa eneo husika na hutafuta ubunifu unaosaidia kujenga sekta husishi na yenye kuwajibika ya madini – pamoja na kuwa na jamii za eneo husika zilizowezeshwa, waamuzi walioelimishwa na uwezo wa kuzingatia haki na majukumu ya wadau wote.

## Kusimulia kuhusu hali ya ubinadamu ya uchimbaji madini ya dhahabu

Ili ielewe vizuri kuhusu watu wote wanaotegemea uchimbaji madini ya dhahabu, IIED ilizuru nchi ya Tanzania ili izungumze na baadhi yao. Kitabu hiki cha picha kinasimulia baadhi ya hali zao. Maonyesho haya yalifadhiliwa na Wakfu wa Ford.

## Hatua zinazofuatia

Maelezo zaidi: www.iied.org/commonground


## Shukrani

**IIED ingependa kuwashukuru wote waliopigwa picha na hasa wale waliosimulia hadithi zao kwa ajili ya mradi huu: Levocatus Saidi Bujiku, Simon Sebastian Nsangano, Fortunatus Wazir, Mlindwa Maganga, Betty Bernard Kakulu, Wellington Moses na familia zao.**

**Tulihuzunika kupata habari za kifo chake Fortunatus Wazir, na tunatuma rambirambi zetu za dhati kwa marafiki zake wote na familia.**

**Mpiga picha:** Brian Sokol/ Panos Pictures.

Wakfu wa Ford





Jina langu ni Levocatus Saidi Bujiku. Nina miaka 22 na nimefanya kazi kama mchimba madini wa kiufundi kwa miaka miwili sasa.

Mimi pia ni mwana, baba na mume. Mwanangu mwenyewe, Kevin, huishi na mama yangu mahali mbali sana. Tumaini langu kubwa ni kumpa elimu ili aweze kunijenga kama mzazi wake. Naomba Mungu niweze kupata pesa za kutosha ili nitunze familia yangu.





Jina langu ni Simon Sebastian Nsangano. Nina miaka 66 na nimekuwa mchimba madini ya dhahabu kwa miaka 50.

Mimi pia ni mkulima na mtu aliye na familia. Ninafanya kazi katika shamba langu kisha kuelekea kwenye migodi yangu ya madini. Mke wangu aliaga hivi majuzi lakini nina watoto wangu wanne. Mimi nina ndoto ya kuipa familia yangu maisha bora. Nafanya kazi kila siku lakini matokeo ni duni sana. Ningelikuwa na pesa ningewapeleka wanangu wote shule ya sekondari.





Jina langu ni Fortunatus Waziri na nina miaka 22. Mwaka wa 2009, nilisafiri kilomita 100 kutoka Kahama hadi Mawemeru; na nimefanya kazi hapa kama mchimba madini wa kiwango kidogo kutoka mwaka huo.


Mimi pia ni baba. Watoto wangu wawili wanaishi na nyanya yangu mbali sana. Mimi huwatumia pesa ninapoweza lakini ni ndoto yangu kupata pesa nyingi niwajengee nyumba. Kama mchimba madini, ninapigania maisha ya watoto wangu usiku na mchana.


February



Jina langu ni Mlindwa Maganga. Nina miaka 41. Mimi ndiye mwenyekiti wa kijiji cha Mawemeru na kama sehemu ya wajibu huo; ninahusika na leseni za viwango vidogo vya uchimbaji madini.

Mimi pia ni mkulima, mchimba madini wa kiwango kidogo, mume na baba. Nina mke na watoto watatu, wa umri wa 13, 7 na 1. Sehemu kubwa ya mapato yangu huenda kwa karo ya shule — Ni muhimu kwangu watoto wangu wapate elimu bora zaidi ili waweze kupata nafasi bora maishani na ulimwenguni.





Jina langu ni Betty Bernard Kakulu. Nina miaka 33 na ninatoka Bukoba, kilomita 300 kaskazini mwa hapa. Nimekuwa wanajiolojia mpatanishi katika mgodi wa dhahabu wa kiwango kikubwa kwa miaka sita na nusu.

Mimi pia ni dada na binti. Asilimia arobaini ya mshahara wangu kila mwezi huenda kuwasaidia ndugu na mama yangu, wanaoishi mbali sana. Nampenda sana mama yangu. Nina ndoto ya kuwa na familia siku moja.





Jina langu ni Wellington Moses. Nina miaka 41 na nimekuwa dereva wa lori la takataka katika mgodi wa kiwango kikubwa kwa karibu miaka kumi. Mimi huendesha lori kubwa zaidi la takataka — tani 250 — nchini Tanzania: ni mtambo waa kuvutia sana.

Mimi pia ni mume na baba. Mimi si maskini wala tajiri; lakini nina kiwango kizuri cha maisha pamoja na mke na watoto wangu watatu. Tumaini langu la maisha ya baadaye ni kwamba watoto wangu wapate elimu ya kutosha.

IIED ni shirika la sera na utafiti wa utekelezaji linalokuza maendeleo endelevu na linalounganisha vipaumbele vya nchini kwenye changamoto za dunia. Afisi zetu ziko jijini London na tunafanya kazi katika bara tano pamoja na baadhi ya watu walioathiriwa zaidi duniani kote ili kuimarisha maoni yao katika majukwaa ya uamuzi yanayowaathiri.


**Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo**

**www.iied.org**

80-86 Gray's Inn Road
London WC1X 8NH, UK

**T :** +44 (0)20 3463 7399 **E :** info@iied.org

www.facebook.com/theIIED

@iied

www.linkedin.com/company/iied


Pakua machapisho zaidi katika www.iied.org/pubs

Nyenzo za mradi